



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA AROBAINI NA NNE – TAREHE 05 JUNI, 2026

I. DUA:

I. KIAPO CHA UAMINIFU NA AHADI YA UZALENDU KWA WABUNGE:

Mhe. Emmanuela Mtatifikolo Kaganda

II. MASWALI:

OFISI YA WAZIRI MKUU (TAMISEMI):

518. MHESHIMIWA KASSIM HASSAN HAJI (MWANAKWEREKWE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali italetwa Marekebisho ya Sheria ili kuondoa changamoto zinazoendelea katika utekelezaji wa Mfuko wa Jimbo.

519. MHESHIMIWA HAMOUD ABUU JUMAA (KIBAHA VIJIJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Barabara ya Kongowe - Soga kwenye *Station* ya Soga kwa kiwango cha lami.

520. MHESHIMIWA BAKARI BAKARI SHINGO (UKONGA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Barabara ya Pugu – Mnadani – Bangulo hadi Ulongoni B.

WIZARA YA KILIMO:

521. MHESHIMIWA ISAYA MOSES MNGURUMI (KONGWA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuanza uchimbaji wa Bwawa la Chilanzilizi Kata ya Ngomai - Kongwa.

WIZARA YA MAJI:

522. MHESHIMIWA SIKUDHANI YASSINI CHIKAMBO (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini Serikali itamlipa Mkandarasi ili kukamilisha Mradi wa Maji Tunduru ambao umesimama.

WIZARA YA UJENZI:

523. MHESHIMIWA GEORGE NATANY MALIMA (MPWAPWA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Daraja la Godegode kwa kuwa Mkandarasi ameshapatikana.

524. MHESHIMIWA HUSNA JUMA SEKIBOKO (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Barabara ya Lushoto, Magamba, Lukozi, Mlalo mpaka Umba *Junction* kwa kiwango cha lami.

WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA:

525. MHESHIMIWA JANETH ELIAS MAHAWANGA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara:-

Je, BRELA inachukua hatua gani kulinda bidhaa za Wanawake dhidi ya wizi wa Nembo, Chapa au Mawazo ya ubunifu.

WIZARA YA FEDHA:

526. MHESHIMIWA TINNAR ANDREW CHENGE (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha:-

Je, Serikali inatumia kigezo gani katika kutoza Kodi ya Majengo (*Property Tax*) kupitia Mfumo wa Mita za Luku nchini.

WIZARA YA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:

527. MHESHIMIWA MASACHE NJELU KASAKA (LUPA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari:-

Je, lini Serikali itajenga Mnara katika Kijiji cha Shoga ili kutatua changamoto ya mawasiliano ya Simu.

WIZARA YA UCHUKUZI:

528. MHESHIMIWA GRACE ELIAS MKOMA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi:-

Je, lini Serikali itajenga Uwanja mkubwa wa Ndege Singida.

529. MHESHIMIWA JOHN STEPHANO LUHENDE (BUKENE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi:-

Je, lini Kampuni ya YAPI MERKEZI wanaojenga Mradi wa SGR Bukene italipa fidia ya Tsh. 2,666,666,666.64 inazodaiwa na Halmashauri ya Nzega.

**DODOMA
05 JUNI, 2026**

**BARAKA I. LEONARD
KATIBU WA BUNGE**